Uhuru, Ijumaa Septemba 12, 2025 Pg 6

# Abiria wafuate taratibu za usafiri 'Treni ya Mwakyembe'



Na REHEMA MOHAMED

KUMEKUWEPO na tabia ya baadhi ya abiria wa Treni ya Mwakyembe kupanda kabla ya treni haijasimama vizuri katika kituo cha Gerezani.

Kitendo hiki ni hatari kwa usalama wa abiria wenyewe, kwani kinaweza kusababisha kuanguka, kujeruhiwa vibaya au hata kupoteza maisha.

Mbali na madhara ya kiafya, tabia hii inaashiria ukosefu wa nidhamu na uvumilivu miongoni mwa baadhi ya abiria, hali inayoweza kusababisha vurugu na usumbufu kwa wasafiri wengine.

Aidha, matukio kama haya hupunguza hadhi ya huduma za usafiri wa reli na kusababisha hofu kwa abiria wapya.

Mfano kumekuwa matukio madogo madogo ya abiria kuumia kutokana na kukanyagwa au kusukumana yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara katika kituo cha Gerezani na maeneo mengine.

Ili kudhibiti kabisa tatizo hili, inapendekezwa kuwepo na adhabu au faini kwa abiria watakaokiuka kanuni za usalama.

Kwa mfano, abiria atakayebainika kudandia treni kabla haijasimama anaweza kutozwa faini ya kati ya shilingi

> **Mfano kumekuwa matukio madogo madogo ya abiria kuumia kutokana na kukanyagwa au kusukumana yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara katika kituo cha Gerezani na maeneo mengine.**

30,000 hadi 50,000 au kunyimwa huduma kwa muda maalumu.

Hatua hii itasaidia kuongeza nidhamu, kuwawajibisha wakiukaji na kulinda maisha ya wasafiri.

Abiria hudandia treni kabla halijasimama vizuri kwa lengo la kuwahi siti, wasafiri wakiwa wamekaa.

Hata hivyo, abiria wanapaswa kuelewa kuwa maisha yao ni ya thamani kuliko siti wanayoikimbilia.

Safari ya kutoka gerezani hadi Pugu kwa usafiri wa treni haizidi saa moja, hivyo si umbali mrefu wa kumfanya mtu kuwahi siti huku akihatarisha maisha yake.

Pia ikumbukwe, abiria wanashuka njiani hivyo upo uwezekano wa kupata siti na kukaa.

Ni muhimu mamlaka husika na viongozi wa usafiri wa reli kuimarisha elimu ya usalama kwa abiria, kusisitiza nidhamu katika vituo, kuweka matangazo ya mara kwa mara kuhusu athari za kupanda treni kabla haijasimama.


Vilevile, askari na maofisa usalama wa kituo waongezewe nguvu kudhibiti mienendo hiyo isiyo salama.

Kwa upande wa abiria, subira na uvumilivu ni silaha pekee ya kuokoa maisha na kuhakikisha kila mmoja anafika anakoenda salama.

CS CamScanner

CS CamScanner

**HATARI** Uhuru, Ijumaa Septemba 12, 2025 pg 16



**LORI lenye shehena ya mizigo bila kuzingatia sheria za usalama barabarani, likiwa limegeshwa kando ya Barabara ya Mlele- Mpanda, katika Kijiji cha Majimoto, mkoani Katavi, juzi.** (Picha na Njumai Ngota).

CamScanner

CamScanner

Mwananchi, IJUMAA, Septemba 12, 2025 Pg3

# Ajali ya Fuso, gari ndogo yaua saba Rorya

Beldina Nyakeke , Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Rorya.** Watu saba wamefariki dunia papo hapo na mmoja kujeruhiwa baada ya gari walikokuwa wakisafiria kugonga kwa nyuma gari lililokuwa limeegeshwa barabarani baada ya kuharibika.

Ajali hiyo ilitokea katika Kijiji cha Buganjo wilayani Rorya wakati gari aina ya Toyota Succeed likiwa limebeba watu saba likiwa linatoka mjini Tarime kuelekea Kijiji cha Busurwa wilayani Rorya, liligonga kwa nyuma gari aina ya Fuso lililokuwa limeegeshwa pembezoni mwa barabara baada ya kuharibika.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Tarime/Rorya, Mark Njera alieleza ajali hiyo imetokea jana saa 11 alfajiri.

"Gari aina ya Succeed iliyokuwa inatoka Tarime kuelekea Rorya iligonga kwa nyuma gari aina ya Fuso lililokuwa limeegeshwa pembezoni mwa barabara baada ya kuharibika," alisema Kamanda Njera.

Alisema majina ya watu hao hayajatambulika na miili yao imehifadhiwa katika Hospitali ya Utegi wilayani Rorya huku hali ya majeruhi ikiwa ni mbaya.

Kamanda Njera alisema Jeshi la Polisi limeanza uchunguzi ili kubaini chanzo cha ajali hiyo. Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo walidai chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa madereva wote wawili ikiwamo mmoja kuegesha gari bila kuweka alama ya tahadhari.

"Huyu dereva wa gari dogo naye inaonekana alikuwa mwendo kasi hakuchukua tahadhari na mbaya zaidi amehama upande wake kwenda wa pili sasa ile anashtuka tayari ameparamia fuso," alisema Bernard Okos.



Askari polisi wakiangalia mabaki ya gari ndogo iliyopata ajali eneo la Ahaki katika Kijiji cha Buganjo wilayani Rorya jana. **Picha na Beldina Nyakeke**

Aliwaomba madereva kuwa makini na kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepuka athari za ajali zinazoweza kuzuilika.

Godfrey Godfrey alidai watu hao ni wafanyabiashara wa dagaa na walikuwa wakielekea kwenye shughuli zao katika Mwalo wa Busurwa wilayani Rorya.

Ajali hiyo imetokea ikiwa imepita takribani miezi miwili tangu ajali iliyoua watu wanne na wengine wanne kujeruhiwa kutokea katika Kijiji cha Mtegu mkoani Lindi baada ya kugongwa na lori la mizigo lililokuwa likisafirisha makaa ya mawe.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, John Imori alisema lori hilo likiwa na mzigo wa makaa ya mawe, baada ya kufika kwenye mteremko katika Kijiji cha Mtegu lilitoka pembezoni mwa barabara likiwa kwenye mwendo kasi na kuwagonga watu zaidi ya 10.

"Chanzo cha ajali hiyo, gari liliacha njia likiwa kwenye mwendo kasi na kisha kuelekea upande wa kulia na kuwagonga watu waliokuwa maeneo hayo na kusababisha vifo vya watu wanne," amesema Kamanda Imori.

Ajali hiyo ilitokea Juni 27, mwaka huu saa moja usiku baada ya kufika kwenye mteremko.

CamScanner
CamScanner